

NENO LA UTANGULIZI KUTOKA KWA BW. LAWRENCE MAFURU,  
KATIBU MTENDAJI WA TUME YA MIPANGO, WAKATI WA  
KUFUNGUA WARSHA ELEKEZI YA TIMU YA WATAALAMU YA  
MAANDALIZI YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO, 2050

TAREHE 13 JANUARI 2024, UKUMBI WA GOLDEN TULIP ZANZIBAR  
AIRPORT HOTEL (ZANZIBAR)

---

*Mhe. Prof. Kitila Alexandra Mkumbo (Mb) - Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais  
Mipango na Uwekezaji;*

*Dkt. Tausi Kida - Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji;*

*Wajumbe wa Timu ya Wataalam ya Uandishi wa Dira ya Taifa ya  
Maendeleo 2050;*

*Wajumbe wa Sekretarieti ya Maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo  
2050;*

*Washiriki wa Warsha Elekezi.*

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA**

*Ndugu Mgeni rasmi*

Awali ya yote nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo. Vile vile niwakaribishe katika Warsha hii Elekezi ya Wajumbe wa Timu ya Wataalamu ya Uandishi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Kwa baadhi yenu zoezi hili siyo geni kwani mlibahatika kupitishwa kwenye warsha inayofanana na hii wakati mchakato wa maandalizi ya Dira ulipokuwa chini ya Wizara ya Fedha.

*Ndugu Mgeni Rasmi*

Lengo la kukusanyika hapa ni kujenga uelewa wa pamoja kwa Timu ya Wataalamu ya Uandishi wa Dira kuhusu mchakato wa maandalizi ya Dira

ya Taifa ya Maendeleo 2050. Tunafanya hivi ili kila mmoja wetu aelewe majukumu atakayo kuwa nayo katika uandaaji wa Dira na kufahamu hatua zote muhimu katika uandishi wa Dira, 2050. Vile vile kwa kuwa baadhi ya wajumbe katika timu hizi kitaaluma sio wanamipango na katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku hawajihusishi na shughuli za mipango ya maendeleo ni vyema tukapata fursa ya kukakaa pamoja na kubadilishana mawazo kabla ya kuanza rasmi kutekeleza majukumu yaliyo mbele yetu.

*Ndugu Mgeni Rasmi*

Katika warsha hii, wajumbe watajengewa uelewa kwenye masuala mbalimbali ikiwemo: Dhana kuhusu mipango ya maendeleo; Historia ya Mipango ya maendeleo tangu nchi ipate uhuru mwaka 1961; Mchakato wa maandalizi ya Dira 2050; taarifa mbalimbali ambazo zimekwisha andaliwa kwa ajili ya kutumika katika maandalizi ya Dira ikiwemo taarifa ya tathmini ya Dira 2025; shughuli ambazo zimeshafanyika na zinazotarajiwa kufanyika katika maandalizi ya Dira; na Majukumu ya wajumbe wa Timu ya Wataalam ya Uandishi wa Dira, 2050.

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

Ni matumaini yangu kuwa mwisho wa warsha hii elekezi wote tutakuwa kwenye ukurasa mmoja wa namna tutakavyotekeleza jukumu lililoko mbele yetu la kuandaa Dira ya taifa ya Maendeleo ya 2050. Vile vile ni matarajio yangu kuwa baada ya warsha hii kila mmoja wetu atakuwa tayari kutekeleza majukumu yake ili kupata Dira iliyo bora na yenye maono ya Watanzania kwa miaka 25 ijayo.

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

Naomba sasa nichukue fursa hii kumkaribisha Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Zanzibar, ili aweze kutoa maelezo mafupi ya namna Zanzibar itakavyoshiriki katika mchakato wa maandalizi ya Dira 2050.